WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Chuo cha Ualimu Kabanga,
S. L. P. 265,
KASULU.
KIGOMA

SIMU: 0767-317582/ 0715-317582
E-Mail Kabangatc@gmail.com
Kumb. Na. KBCCU/GFO/186/XI/

20/08/2018

Bw/Bi_____
_____

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU ASTASHAHADA YA ELIMU MSINGI NA ELIMU YA AWALI CHUO CHA UALIMU KABANGA MWAKA WA MAFUNZO 2018/2019

1. UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Astashahada ya Elimu Msingi au ELIMU YA AWALI kwa mwaka wa masomo **2018/2019**. Hongera sana!. Mafunzo haya yatachukua muda wa miaka miwili (02), kuanzia **Oktoba 2018**. Unatakiwa kuripoti Chuoni tarehe **04.10.2018**. Nakutahadharisha kuwa ukiripoti Chuoni baada ya Tarehe **17.10.2018 hutapokelewa.** Nafasi yako itajazwa na waombaji wa akiba.

2. MAHALI CHUO KILIPO:

Chuo Cha Ualimu Kabanga kipo Mkoa wa Kigoma Wilaya ya Kasulu.
Chuo kipo km. 7 upande wa Kaskazini mwa mji wa Kasulu.
Kuna usafiri wa mabasi makubwa na madogo toka Manispaa ya Kigoma Ujiji kwenda Kasulu na usafiri wa mabasi madogo (Daladala) toka Kasulu Mjini kuja Kabanga. Ukifika Kasulu Mjini, uliza kituo cha daladala za kuja Kabanga.

Tanbihi: Kwa wale watakaopitia Kahama, panda magari yanayokuja Kigoma - Kasulu.
Usipande magari yanayokwenda Kabanga, kuna Kabanga nyingine Wilaya ya Ngara-Kagera.

- Dira ya Chuo: Kupata Mwalimu Bora
- Kauli mbiu: Elimu Bora.

3. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI:-

i) Cheti halisi cha kuzaliwa na kivuli chake (photocopy)
ii) Cheti halisi chenye picha iliyogongwa Muhuri wa shule cha kumaliza kidato cha nne (Secondary School Leaving Certificate) na kivuli chake (photocopy)
iii) Original Result Slip kwa wale waliomaliza shule mwaka 2017, na Cheti halisi cha taaluma cha kidato cha nne kwa wale waliomaliza nyuma ya mwaka 2017 kilichotolewa na Baraza la Mitihani na kivuli chake (photocopy-2). **Usije na matokeo yaliyotolewa kivuli toka kwenye kitabu cha matokeo ya mtihani**.
iv) Kitambulisho cha shule ya sekondari au Kitambulisho cha mpiga kura/Bima ya afya.

Tanbihi: Kama umefanya mtihani zaidi ya mara moja, uje na vyeti vyote, na kama umefanya mtihani wa Kidato cha sita hukufaulu vizuri, uje na cheti hicho.

v) Uje na barua hii ya maelekezo (Joining Instructions) wakati wa kuripoti Chuoni.
vi) Unatakiwa ujitegemee kwa usafiri wa kuja Chuoni na wakati wa likizo.

4. <u>ADA NA MICHANGO:</u>

Unatakiwa kulipa ada na michango kama ifuatayo:-

1. Ada ya Mafunzo	600,000/= kwa mwaka au 300,000 kwa muhula
2. Huduma ya kwanza kwa kila mwaka	5,00/=
3. Bima ya Afya ya Taifa kwa wale wasio na Bima ya Taifa kwa kila mwaka	50,400/=
4. Usajili mara moja mwaka wa kwanza	5,000/=
5. Serikali ya Wanachuo kwa kila mwaka.	5,000/=
6. Kukodi Godoro kwa kila mwaka	20,000/=
7. Tahadhari kwa kila mwaka	20,000/=
8. Kitambulisho kwa mwaka wa kwanza.	5,000/=
9. Elimu ya Michezo kwa kila mwaka	10,000/=
10. Ulinzi kwa kila mwaka	15,000/=
11. ICT kwa kila mwaka	20,000/=
12. T-Shirt yenye Nembo ya Chuo kwa mwaka wa kwanza	15,000/=
13. Taaluma kwa kila mwaka	50,000/=
14. Usafi na miundombinu kwa kila mwaka.	20,000/=
15. Ada ya mtihani wa Taifa, inaweza kulipwa mwaka wa pili.	50,000/=

<u>NB;</u> Ada ilipwe kupitia Akaunti ya Chuo **NMB KASULU**. Jina la Akaunti: **KABANGA TEACHERS' COLLEGE – REVENUE COLLECTION ACCOUNT. A/N. 51401100003.**

Na Michango ilipwe kupitia Akaunti maalumu ya Chuo**. NMB KASULU.**

Jina la Akaunti**: KABANGA TEACHERS' COLLEGE - MAENDELEO ACCOUNT. A/N. 51403500086.**

<u>ANGALIZO:1</u>. Hakikisha unamweleza mpokea fedha wa benki (Bank Teller) kuwa fedha uliyoweka ni ya Ada au ya Michango na aandike Jina sahihi la Mwanachuo anayelipiwa kwenye "Bank-pay-in-Slip" sehemu ya Saini ya mwenye Akaunti.

2. Ili kuepuka Usumbufu, kila fedha ilipwe kupitia Akaunti husika.
   Bank-pay in-Slip izalishwe kivuli (photocopy) nakala moja ya kwako na nakala ya pili ofisi ya usajili na nakala halisi ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Chuo mara ufikapo Chuoni.
3. Ni lazima kulipa Ada yote au nusu yake (muhula mmoja) na michango yote.
   Zingatia maelekezo kinyume na hivyo hutasajiliwa kuanza masomo.

5. <u>VIFAA MUHIMU:</u>

Uje na vifaa vifuatavyo:-

- Shuka 2 za rangi ya Pinki (zisiwe na maua).
- Blanketi 1.
- Mto na Foronya ya Pinki.
- Chandarua ni lazima kuna mbu wengi wakati wote.
- Ndoo na beseni kwa ajili ya kuhifadhia maji na kufanyia usafi.
- Mopa 1, Hardbroom 1, Fyekeo 1, Reki 1, Jembe na mpini wake.
- Vyombo vya kulia chakula yaani sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
- Gumboots wakati wa mvua kuna tope jingi.
- Vifaa vya michezo Bukta/Sketi,/track-suit rangi ya light-blue, jozi ya raba na soksi ndefu rangi nyeupe au bluu.

Usipoleta vifaa vilivyotajwa hapo juu hutasajiliwa.

6. <u>SARE YA CHUO:</u>

<u>WAVULANA:</u>

i) Suruali mbili (2) rangi nyeusi, za kushonwa zenye mfuko mmoja nyuma na rinda mbili kila upande.
ii) Tai ndefu rangi nyeusi ifike unapovalia mkanda wa suruali**.**
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba.
iv) Mkanda mweusi wa kuvalia suruali.
v) Mashati mawili (2) rangi ya **bluu bahari mapya**.
Atakayependa kuvaa koti lazima lifanane na rangi ya suruali.

WASICHANA:

i) Mashati mawili (2) rangi ya **bluu bahari mapya.**

ii) Sketi mbili za rangi nyeusi **(Kitambaa kizito**) zenye mashono ya rinda boksi inayovuka magoti kwenda chini.na ziwe za heshima.

iii) Tai fupi ya rangi nyeusi itakayoishia chini ya kitovu.

iv) Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi vya kufunga Kamba.

v) Soksi nyeupe ndefu. (Stockings).

vi) Wanachuo Waislamu wataruhusiwa kuvaa juba inayofanana na rangi ya shati.

Tanbihi: * Uje na nguo za heshima.

* Usije na Masanduku/mabegi makubwa, hatuna nafasi ya kuyaweka. Ukija nalo itabidi ulirudishe nyumbani.

* Simu za mkononi **haziruhusiwi** kutumika katika vyumba vya madarasa, mtihani, wakati wa kujisomea jioni (Prep). katika mkutano wa Chuo, wakati wa kazi za mikono, michezo na katika shughuli zote rasmi za Chuo.

7. TAALUMA:

Uje na vifaa vifuatavyo:-

i) Daftari (counter books) za kutosha, zipatazo 14.

ii) Kalamu za wino za kutosha muhula mzima.

iii) Rula, mathematical set moja na penseli.

iv) Karatasi ya photocopy ream **02 (Double A)** kwa mwaka. (Atakayeleta tofauti na hiyo atalazimika kununu nyingine).

8. MITIHANI:

Chuo hutoa mitihani. Unatakiwa ufaulu mitihani yote itakayotolewa na Chuo na utaachishwa mafunzo endapo utaonekana dhaifu katika mitihani hiyo.

9. AFYA:

Chuo hakitagharamia matibabu ya mwanachuo wakati wa mafunzo yake. Unatakiwa ulipe fedha kwa ajili ya kupewa Kadi ya Bima ya Afya au Kadi ya Bima ya afya kwa ajili ya matibabu. Kuna hospitali kuu mbili, moja ya Serikali ipo km.7 na nyingine ya shirika la Dini.

Hii ya pili ipo meta chache toka chuoni na inapokea wagonjwa wenye kadi za Bima ya afya.

Kabla ya kuripoti Chuoni hakikisha unapimwa afya yako na mganga mkuu **wa Hospitali ya Serikali kuthibitisha kama afya yako inakuruhusu** kuchukua Mafunzo ya Ualimu.Wajawazito hawatapokelewa. Aidha Chuo hakina huduma ya chakula maalum (special-Diet) kwa wanachuo wenye matatizo ya chakula.

Tunashauri wale wanaohitaji aina ya huduma hiyo waahirishe mafunzo.

10. KANUNI ZA CHUO:

- Mwalimu ni mfano mzuri wa kuigwa na jamii. Chuo kinakutarajia kuwa na sifa za mwalimu utakapoingia chuoni na Kumaliza mafunzo yako. Kanuni za chuo utazikuta chuoni.
- Utapitishwa katika sheria na taratibu zote za Chuo mara ufikapo Chuoni. Aidha utapewa fomu ya kujaza kukubaliana na sheria na taratibu hizo.

11. MWISHO

Nakutakia maandalizi mema, zingatia sana maelekezo yaliyotolewa.

Nakutakia kila la kheri na **KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU KABANGA**.

SULEIMAN H. KAMBI

KAIMU MKUU WA CHUO

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMIN

To: The Medical Officer

From: Kabanga
Teachers` College

……
……..
Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.
A: 1. (a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group.
Date:…….Signature……

Official Stamp

PART B: MEDICAL CERTFICATE
(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named student that he/she is physically fit/ unfit and mentally *fit/ unfit for a full time teacher Education course
(a) Eye-sight……
(b) Hearing……
(c) Speech……
(d) Venereal Diseases……
(e) Leprosy……
(f) Limbs……
(g) Epilepsy……

II. Neuroses……
III. Otherseriousdiseases……
IV. Pregnancy……

Date:……Signature……..

Official Stamp